

# Uchunguzi wa saratani ni nini?

Uchunguzi ni sehemu muhimu ya kutunza afya yako



Uchunguzi wa saratani unahusisha vipimo vya rahisi vinavyotafuta dalili za mwanzo wa saratani, au hali zinazosababisha saratani. Vipimo vya uchunguzi vinaweza kugundua saratani kabla wewe kujisikia mabadiliko yoyote ya mwili wako. Wakati unapogundua saratani mapema, ni rahisi kutibu kwa mafanikio. Nchini Australia, kuna miradi mitatu ya kitaifa ya uchunguzi. Hizi ni kwa saratani za matiti, matumbo na za mlango ya uzazi.



## Uchunguzi wa matiti



Saratani ya matiti ni saratani ya kawaida zaidi katika wanawake

- Wanawake wa umri wa miaka 50 hadi 74 wanapaswa kupata mammogram (inayoitwa pia eksrei ya matiti) kila miaka miwili.
- Mammogram ni njia bora ya kugundua saratani ya matiti kabla ya kuonekana au kuhisiwa.
- Ni muhimu kwa wanawake wote wa umri wa miaka 50 hadi 74 kuchunguzwa, kwa sababu wanawake wengi wanaogunduliwa na saratani ya matiti hawana historia ya familia ya ugonjwa huu.
- Mammogram inayofanywa na BreastScreen NSW ni **bure**. Mwelekeo wa daktari hauhitajika.



### Kile cha kufanya:

- Kupanga miadi piga simu kwa **13 20 50** au tembelea [book.breastscreen.nsw.gov.au](http://book.breastscreen.nsw.gov.au)
- Piga simu kwa **13 14 50** ili kuongea na mkalimani.
- Kwa habari zaidi katika lugha nyingine, tembelea [breastscreen.nsw.gov.au](http://breastscreen.nsw.gov.au)



## Uchunguzi wa matumbo



Saratani za matumbo 9 kati ya 10 zinaweza kutibiwa kwa mafanikio ikiwa zinagunduliwa mapema

- Wanaume na wanawake wa umri wa miaka 50 hadi 74 wanao kadi ya Medicare au ya Department of Veterans Affairs wanatumwa kifaa **bure** cha uchunguzi wa matumbo kwa posta kila miaka miwili.
- Uchunguzi wa saratani ya matumbo ungeweza kuokoa maisha yako, kwa sababu ni njia bora ya kugundua saratani ya matumbo mapema.
- Kipimo cha chunguzi wa saratani ya Matumbo ni upesi na rahisi kufanya nyumbani kwako mwenyewe.



### Kile cha kufanya:

- Tumia kifaa chako cha uchunguzi wa matumbo wakati kinapofika kwa posta.
- Tembelea [dothetest.com.au](http://dothetest.com.au) kuangalia wakati kifaa chako kinachofuata kitakapotumwa kwako.
- Piga simu kwa **1800 627 701** kwa maswali mengine yote.
- Piga simu kwa **13 14 50** ili kuongea na mkalimani.
- Kwa habari zaidi katika lugha nyingine, tembelea [health.gov.au/resources/translated](http://health.gov.au/resources/translated)



## Uchunguzi wa mlango wa uzazi



Uchunguzi wa mlango wa uzazi unaweza kuzuia saratani ya mlango wa uzazi

- Wanawake wa umri wa miaka 25 hadi 74 wanapaswa kupata uchunguzi wa mlango wa uzazi kila miaka mitano.
- Unaweza kupanga Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi na daktari au muuguzi wa mtaa wako.
- Madaktari wengine wanatoa huu **bila malipo**. Unaweza kuuliza kuhusu gharama wakati unapopanga miadi.
- Saratani ya mlango wa uzazi inaweza kuzuia kwa kupata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi. Hii ni kwa sababu inatafuta kwa maambukizi inayoitwa human papillomavirus (HPV), ambayo inasababisha saratani ya mlango wa uzazi.



### Kile cha kufanya:

- Piga simu kwa **1800 627 701** kuangalia wakati unapofaa kwa Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi.
- Panga miadi na daktari au Muuguzi. Unaweza kuomba kwa daktari au muuguzi wa kike kufanya kipimo.
- Piga simu kwa **13 14 50** kuongea na mkalimani.
- Kwa habari zaidi, tembelea [cancer.nsw.gov.au/cervical](http://cancer.nsw.gov.au/cervical) or [cancerscreening.gov.au/cervical](http://cancerscreening.gov.au/cervical)